# MTIHANI WA KARAMA ZA KIROHO KWA WATU WAZIMA

**Maagizo:**

Warumi 12:3 inasema, "Kutokana na neema aliyonijalia Mungu, nawaambieni nyinyi nyote: Msijione kuwa ni kitu zaidi kuliko mnavyopaswa kuwa. Fikira zenu na ziwe na kiasi kadiri ya kipimo cha imani Mungu aliyomgawia kila mmoja."

Ili kupata matokeo bora zaidi, jibu kila kauli kulingana na sifa ulizonazo, sio sifa ambazo ungetaka kuwa nazo ama unazofikiria unastahili kuwa nazo. Je, kauli hizi ni za ukweli kwa kiwango gani? Je, uzoefu wako umekuwa upi? Je, watu wengine wanakuambia nini? Je, kauli hizi zinaashiria jinsi unavyoyaishi maisha yako ya kila siku kwa kiasi gani? Kila swali ni muhimu, kwa hivyo jaribu kujibu maswali yote. Utahesabu alama utakazopata mwishoni mwa mtihani.

**Jibu kila kauli kulingana na kipimio cha pointi 1-5 kifuatacho:**
**1 = Sio Sahihi Kabisa**
**2 = Sio Sahihi Kwa Kiasi**
**3 = Sio Sahihi Wala Sahihi**
**4 = Sahihi Kwa Kiasi**
**5 = Sahihi Kabisa**

---

## Anza:

1. _______ Nina ujuzi wa kupanga watu ili kutimiza malengo au kazi nyingi tofautitofauti.

2. _______ Ninataka kuanzisha na kutayarisha makanisa na/au huduma mpya.

3. _______ Ninaweza kugundua kwa urahisi kama kauli imetolewa kwenye Biblia au la.

4. _______ Ninaweza kuhubiria watu wengine injili kwa uwazi na ufanisi.

5. _______ Nina azimia kuwahamasisha watu wengine wanaopitia wakati mgumu katika imani yao.

6. _______ Ninaishi kwa ujasiri nikijua kuwa Mungu ananijali na kujihusisha na maisha yangu kwa undani.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

7. _______ Ninaishi mtindo wa maisha rahisi ili niweze kutoa fungu kubwa zaidi la mapato yangu kwa kazi ya Mungu.

8. _______ Mara nyingi watu huniuliza mtazamo au ufafanuzi wangu wa mistari hususa ya Biblia.

9. _______ Watu wengine hufuata uongozi wangu.

10. _______ Nina hisia-mwenzi kubwa kwa wale wanaopambana na mambo magumu katika maisha yao.

11. _______ Ninalinda sana maslahi ya kiroho ya watu wengine.

12. _______ Wakati mwingine Mungu amenipa ujumbe kwa mtu binafsi au kundi la watu na kunipa msukumo niwafikishie ujumbe huo.

13. _______ Ninafurahi kufanya majukumu ya kila siku yanayosaidia huduma tofautitofauti kanisani.

14. _______ Ninatumia muda mwingi kusoma Neno la Mungu kwa kujua kuwa bidii yangu italeta mabadiliko katika maisha ya watu.

15. _______ Mara nyingi huwa nina maarifa yenye msaada kunapokuwa na hali ambazo hazijadhihirishiwa watu wengine.

16. _______ Ninaweza kuona kwa urahisi kinachofaa kufanywa na kutekeleza mipango ili kuleta mafanikio.

17. _______ Mipaka ya kiutamaduni haizuii kazi yangu ya kupanua ufalme wa Mungu.

18. _______ Niko makini kwa mambo yale watu wanayoyasema, jinsi wanavyoyasema, hasaa wale wanaofunza.

19. _______ Ninahisi nina mzigo wa huruma kwa wale waliopotea bila Yesu.

20. _______ Watu wanapovunjika moyo, huwa nawakumbusha kuhusu nguvu na ahadi za Mungu zilizo kwenye Biblia.

21. _______ Ninaamini Mungu atajibu maombi yangu kulingana na mapenzi yake makamilifu.

22. _______ Ninafurahi kutoa mapato yangu mara kwa mara – mara nyingi kuliko fungu la kumi.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

23. _______ Roho ameniletea habari akilini ambayo nimeweza kutumia kuhudumia wengine kwa ufanisi.

24. _______ Nina maono kwa kanisa au huduma yangu na najua kinachostahili kufanywa ili kuyatimiza.

25. _______ Ninawaona wagonjwa na maskini kama watu wanaohitaji zaidi upendo na faraja Yesu anazotupa.

26. _______ Ninapenda kutumia muda nikikuza  na kuelekeza  watu wengine katika imani yao.

27. _______ Kumekuwa na wakati ambapo nimepokea ufunuo kutoka kwa Mungu na nikawaambia watu kanisani.

28. _______ Ninajitolea kwa urahisi kusaidia kanisani ninapojua itatimiza haja fulani.

29. _______ Ninazungumza kuhusu Biblia kwa ufanisi na kwa njia zinazoshawishi na kuhimiza watu wengine kujifunza zaidi.

30. _______ Nimejifunza kupitia uzoefu wangu maishani na mara kwa mara ninaweza kuelekeza watu wengine wanaopitia shida ambazo nimewahi kuzipitia.

31. _______ Mimi ni bora katika kukabidhiana majukumu na ninaamini watu "wafanye kazi zao."

32. _______ Ninaweza kuhudumia watu wa tamaduni tofauti kwa ufanisi.

33. _______ Mimi ni jaji mwenye uepesi na usahihi wa kujua tabia za watu.

34. _______ Nina tafuta njia za kujenga uhusiano na watu wasio Wakristo ili kushiriki Injili nao.

35. _______ Nina shurutishwa kushawishi ukuaji kwa wale ambao imani yaoimesimama.

36. _______ Ninajua Mungu atanisaidia hata kama sioni suluhisho kwa tatizo langu.

37. _______ Ninapotoa ninafurahi kujua kuwa watu zaidi watahudumiwa na kuguswa na Injili.

38. _______ Ninasoma Biblia mara kwa mara ili kushiriki ukweli na watu wengine ndani na nje ya kanisa.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

39. _______ Siogopi kuchukua tahadhari ili kuendeleza ufalme wa Mungu kupitia kanisa au huduma yangu.

40. _______ Ninajali sana kuhusu watu wanaoumia na ninataka kuwasaidia wanapopitia wakati mgumu.

41. _______ Ninatamani kusaidia walioumia na kupotea wapate uponyaji na makao ndani ya Yesu Kristo.

42. _______ Mungu amenipatia taarifa kuhusu mtu nikahisi nina wajibu wa kumkabili ili kumrudisha kwa Mungu.

43. _______ Ninapenda kumhudumia Mungu "bila kujulikana."

44. _______ Ninaweza kueleza ukweli wa kiteolojia kwa undani kwa njia ambayo hata mtoto anaweza kuuelewa.

45. _______ Mara kwa mara mimi husaidia watu kwa kutoa mafundisho na kanuni za Biblia kama suluhisho kwa baadhi ya matatizo ya maisha.

46. _______ Ninapenda kuunda njia zinazofanya mambo yaendeshwe kwa ufanisi katika maisha na kazi yangu.

47. _______ Mungu amenipa ushawishi katika huduma na/au makanisa tofautitofauti.

48. _______ Ninaweza kutambua kwa urahisi ushawishi wa adui au shetani katika hali fulani.

49. _______ Ninapenda kukaliri Neno la Mungu ili kushiriki na wale wasiomjua Yesu kama Mwokozi wao.

50. _______ Mimi siogopi kutoa changamoto kwa mtu ikiwa najua itahamasisha ukuzi wao wa kiroho na ujasiri katika maisha yao.

51. _______ Nitajitokeza kwa ujasiri katika hali ninapohisi Mungu ananiita nifanye hivyo.

52. _______ Ninaamini nimebarikiwa kifedha ili niwe baraka kwa kanisa na umisheni wake wa kufikia waliopotea na kusaidia maskini.

53. _______ Ninakumbuka mengi ya yale ninayojifunza na ninaweza kuyakumbuka kwa upesi panapohitajika.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

54. _______ Ninaweza kutambua viongozi kwa urahisi na ninapenda kuwasaidia kukua katika karama na uwezo wao.

55. _______ Ninapenda kusaidia watu wanapopitia mawimbi ya maisha na kuwaonyesha huruma aliyoonyesha Yesu.

56. _______ Ninajali kuhusu kanisa na ninafanya kadri ya uwezo wangu kuiona ikikua na kujengwa kwa upendo.

57. _______ Mungu ameweka katika mawazo yangu mambo muhimu ambayo awali hayakujulikana ambayo nimetangaza kanisani.

58. _______ Ninatenga muda kila wiki kusaidia wale wanaohitaji msaada kwenye kanisa langu na jamii.

59. _______ Ninapenda kuwasilisha maelezo muhimu ya Neno la Mungu kwa watu wengine.

60. _______ Ninaweza kuona mahali ambako maamuzi na matendo ya mtu binafsi au kundi yatawaelekeza, na ninajitolea kuwaelekeza katika njia inayofaa.

61. _______ Maelezo madogo-madogo ni muhimu kwangu na huwa nina makinika ili kuhakikisha kuwa mambo yanafanywa kwa usahihi.

62. _______ Nimehitimu na ninaweza kuanzisha na kuongoza kanisa au huduma mpya.

63. _______ Mara nyingi ninaweza kugundua ikiwa mtu ni mwingo kabla iwe wazi kwa watu wengine.

64. _______ Ninapenda kushuhudia kuhusu yale Kristo aliyoyafanya katika maisha yangu na jinsi alivyo nisaidia.

65. _______ Watu wengine wameniambia kuwa maneno yangu yamewashurutisha kuondoka na kukua katika imani yao.

66. _______ Hata wakati wa magumu, ninaamini kuwa Mungu atanituliza na kunipa mahitaji yangu.

67. _______ Usimamizi ni sehemu muhimu ya safari yangu ya kila siku na Kristo.

68. _______ Ninapenda kushiriki na watu wengine ukweli na maarifa ambayo Mungu amenionyesha.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

69. _______ Mara nyingi watu hunitegemea kuongoza kikundi au mradi.

70. _______ Ninajulikana "kujali sana" na kusaidia watu wengine wanapohitaji usaidizi.

71. _______ Ninatamani kuona kila mtu kanisani akitimiza kazi kubwa aliyokabidhiwa.

72. _______ Nimepokea kwa ghafla ujumbe kutoka kwa Mungu haswa kwa washiriki wa kanisa letu na nikashiriki nao ili uungwe mkono na kanisa nzima.

73. _______ Ninapoona hitaji kanisani, ninalikidhi bila kuulizwa.

74. _______ Watu wengine wamesema kuwa mafunzo yangu yana manufaa na yanaeleweka kwa urahisi.

75. _______ Naskia kunyenyekea sana wakati mtu anaomba maelekezo yangu, kwa hivyo ninakuwa mwangalifu sana niwasaidie.

76. _______ Ninatumia muda wangu kwa hekima.

77. _______ Ninatamaa ya kiasi cha juu ya kukuza viongozi na wachungaji ambao watatayarisha kanisa.

78. _______ Nina "rada" yenye nguvu ya kugundua mafunzo ya uongo.

79. _______ Siogopi kuwasihi watu waamini kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zao na kumkiri kama Bwana na Mwokozi.

80. _______ Wakati watu wengine wanakabiliwa na matatizo magumu, ninawaambia kwa ujasiri kuhusu uaminifu wa Mungu kwa watu wake.

81. _______ Mara nyingi huwa sina wasiwasi kwa sababu ya imani yangu kwa uwezo wa Mungu na nia yake ya kunisaidia katika kila hali.

82. _______ Ninatafuta njia za kuwasaidia watu wengine kifedha na kushiriki upendo wa Kristo nao.

83. _______ Ninaweza kuhusisha ukweli na hali halisi ya Injili na kila kipengee cha maisha.

84. _______ Siogopi kujitokeza na kushika usukani katika hali tatanishi.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

85. _______ Ninatafuta wale wanaoonekana kama "watu waliopotea" na kuwasaidia kuendeleza maisha yao.

86. _______ Injili ya Yesu Kristo ndicho kitu muhimu zaidi katika maisha yangu na huduma.

87. _______ Watu wengine wamesema kuwa Mungu amewazungumzia kwa uwazi na moja kwa moja kupitia ujumbe nilioshiriki nao.

88. _______ Ninaamini kuna umuhimu wa milele katika kufanya kazi na huduma za kilimwengu.

89. _______ Ninapenda kugundua jinsi Injili ilivyofumwa kwenye Biblia nzima ninapoendelea kutumia muda kuisoma.

90. _______ Ninaweza kuona kwa urahisi ni mpango ama mbinu gani bora zaidi katika hali fulani.

91. _______ Meza yangu au mkusanyiko-kazi wangu umepangwa hivi kwamba ninaweza kufikia ninachohitaji kwa urahisi.

92. _______ Mara nyingi wachungaji na viongozi wengine huja kwangu niwape usaidizi na mwongozo.

93. _______ Watu wengine wameniambia kuwa maono yangu au hukumu langu kwa watu wengine, halim au kauli yameonekana kuwa ya kuaminika.

94. _______ Mengi ya mazungumzo yangu na watu wasio Wakristo huniongoza kuzungumza kuhusu imani yangu katika Yesu.

95. _______ Ikiwa mtu anajikwaza au anaondoka kutoka kwa maisha ambayo Mungu amewakusudia, nitaongea na kuwahimiza kuyakumbuka na kuyarudia maisha yenye raha ndani ya Kristo.

96. _______ Mara kwa mara huwa ninawahimiza watu wengine kumwamini Mungu katika kila jambo.

97. _______ Mimi hutoa kwa ukarimu bila kujifanya kwenye huduma ya watu wa Mungu.

98. _______ Ninaweza kukumbuka mstari au fungu la Biblia linalolingana na hali fulani.

99. _______Mimi ni "mwonaji" zaidi ya nilivyo wa kushughulikia maelezo madogo-madogo. Huwa ninakaza fikira zaidi kwenye picha kubwa kuliko kwenye maelezo ya kila siku.

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.

100. _______ Watu wengine wameonyesha shukrani kuwa nimewatuliza na kuwahudumia katika wakati waliokuwa chini maishani mwao.

101. _______ Huwa ninasaidia watu wengine wawe kama Yesu.

102. _______ Ninaweza kukumbuka mara ambazo Mungu alinipa ujumbe hususa kwa Kanisa lake kupitia mimi.

103. _______ Ninapata furaha kuwa msaidizi na kusaidia wengine katika huduma zao.

104. _______ Mara nyingi Roho Mtakatifu hunipa maneno yafaao ya kusema wakati ninapofundisha mtu binafsi au kikundi.

105. _______ Mara nyingi ninaweza kuona katikati mwa hali tatanishi au ugomvi na kutoa suluhisho mwafaka la kibiblia katika hali hiyo.

## Maelezo Ya Kupata Alama:

A Ndika alama zako (kutoka 1-5) za kila swali kwenye sanduku lenye nambari ya swali hilo. Jumlisha kila safu na uandike alama zako za jumla juu ya ishara ya karama mwafaka. Baada ya kufanya hivyo, unaweza kuangalia ufungu ufuatao ili uone ni karama gani ya kiroho inayosiamamiwa na kila ishara. **Alama ya juu zaidi ya karama yoyote ni 35**. Jinsi alama ilivyo juu, ndivyo ulivyo imarika katika karama hiyo ya kiroho kulingana na majibu yako. Alama ya **29 au zaidi** katika karama yoyote ni isara yenye nguvu ya kuwepo kwa karama hiyo katika maisha yako. Alama za kati ya **22 na 28** zinaweza kuashiria karama ya kiroho iliyo kwenye hatua ya "mche", hasaa ikiwa mojawapo au zaidi ya alama zako tatu za juu zaidi zipo kwenye ukakaya huu.

## Matriki ya Alama:

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com. All rights reserved.

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 31 | 32 | 33 | 34 | 35 | 36 | 37 | 38 | 39 | 40 | 41 | 42 | 43 | 44 | 45 |
| | 46 | 47 | 48 | 49 | 50 | 51 | 52 | 53 | 54 | 55 | 56 | 57 | 58 | 59 | 60 |
| | 61 | 62 | 63 | 64 | 65 | 66 | 67 | 68 | 69 | 70 | 71 | 72 | 73 | 74 | 75 |
| | 76 | 77 | 78 | 79 | 80 | 81 | 82 | 83 | 84 | 85 | 86 | 87 | 88 | 89 | 90 |
| | 91 | 92 | 93 | 94 | 95 | 96 | 97 | 98 | 99 | 100 | 101 | 102 | 103 | 104 | 105 |
| **Jumla ya Alama** | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Ishara za Karama** | **Ad** | **Ap** | **Di** | **Ev** | **Ex** | **Fa** | **Gi** | **Kn** | **Le** | **Me** | **Pa** | **Pr** | **Se** | **Te** | **Wi** |

## Ishara za Karama:

**Ad** = Usimamizi

**Ap =** Utume

**Di** = Hekima

**Ev** = Uinjilisti

**Ex** = Kuhimiza

**Fa** = Imani

**Gi** = Kupeana

**Kn** = Maarifa

**Le** = Uongozi

**Me** = Huruma

**Pa** = Mchungaji

**Pr** = Kutabiri

**Se** = Huduma

**Te** = Kufundisha

**Wi** = Busara

Copyright © 2017 www.SpiritualGiftsTest.com.  All rights reserved.